



Mwanzo wa Mafunzo
Hudumaya
Christians Sharing Christ

'Kisayi Mwanzo - Kifaa ya kifaa'

SWRland

Aniay Kifaa • Aniay Kifaa • Aniay Kifaa • Aniay Kifaa

TUNAVYOAMINI

Washirka wenza wanathibitisha na kuamini ukawaida wa imani yao katika yafuatayo:

1. Tunaamini katika maandika ya Biblia Takatifu (Agano la Kale na Agano Jipya kwamba, imeandikwa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, na haina makosa katika kuandikwa kwake tangu mwanzo, na kwamba maandiko yaliyomo ndani yake, yana nguvu na yanamamlaka ya mwiso katika imani na uzima.
2. Tunaamini katika Mungu mmoja, aliyefunuliwa katika nafsi tatu: Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu.
3. Tunamwanini Yesu ni Mungu, Bwana wetu, aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na bikira Mariamu, akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulubiwa, akafa, akazikwa, akashuka mahali pa wafu; siku ya tatu akafufuka, akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa mungu Baba Mwenyezi, kutoka huko atakuja kuwashukumu walio hai na wafu.
4. Tunaamini kuwa wokovu unajumuisha ondoleo la dhambi, unaosababishwa na matendo ya haki ya Kristo na karama za uzima wa milele zinazopokelewa kwa imani pekee. Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, watu wote walihesabiwa dhambi na kwa sababu hiyo wanahitaji kuokolewa na nguvu ya Roho Mtakatifu.
5. Tunaamini katika "Ulinzi wa milele" wa waaminio; kuwa hakuna hata mmoja aliyezaliwa katika familia ya Mungu atakayepotea.
6. Tunaamiini kuwa utakaso wa kimaandiko wa kanisa ni ubatizo na meza ya Bwana na kuijunga na kanisa la mahali, tunaamini kuwa ubatizo wa kuzamisha ni lazima utolewe kwa waaminio kama ishara ya kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo, na kuwa meza ya Bwana ni kwa wale waliobatizwa tu kukumbuka kifo chake mpaka atakaporudi tena.
7. Tunaamini katika ufufuo wa mwili kwa mwenye haki na asiye haki, Baraka za milele kwa waliookolewa na hukumu ya milele kwa walipotetea.
8. Tunaamini kwamba Christo aliliagiza kanisa kwenda ulimwenguni kote na kuhubiri Injili kwa kila mmoja, kuwabatiza na kuwafundisha wale wanaoamini.

KUMBUKA: Huduma ya CSCFM ni huduma inayofanya kazi na madhehebu yote yanayoamini na kuukubaliana katika yale tunayoamini hapo juu.

YALIYOMO

Tunavyoamini	2
Yaliyomo	3
Utangulizi	4
Faida za Uinjilisti wa kutumia sinema	5
Matayarisho na upangaji	7
Kuomba Kibali cha Onesho la Cinema	9
Kufundisha timu yako	10
Onesho la Cinema	14
Ufuatiliaji	16
Utunzaji wa kumbu kumbu	17
Maelekezo ya ujazaji wa Taarifa	19
Kiambatanisho na.	
1 Tovuti ya CSCFM	21
2 Eneo la kuingilia mmisheni	21
3 Eneo la Mmisheni	22
4 Kujaza taarifa ya huduma ya mmisheni	22
5 Taarifa ya Mwaka ya huduma ya Mmisheni	23
6 Mwongozo wa mafunzo	23
7 Matumizi ya mtandao kwa baadaye	24
8 Ripoti ya timu za CSCFM kwa mwaka	25
9 Ramani kanda 1	26
10 Ramani kanda 2	27
11 Mambo ya Msingi katika kufunga onesho 1	28
12 Mambo ya Msingi katika kufunga onesho 2	30
13 Mambo ya Msingi katika kufunga onesho 3	31
14 Mfano wa kujitambulisha kwanye uongozi	32
15 Mfano wa shuhuda	33
16 Orodha ya vifaa vya kuuneshea cinema	34
17 Mwongozo wa kufuata katika onesho la cinema	36
18 Kadi za ufuatiliaji	38
19 Mfano wa Tangazo la cinema ya CSCFM	39
20 Taarifa ya kila mwezi ya huduma ya CSCFM	40
Makubaliano ya utunzaji wa vifaa vya huduma	41

UTANGULIZI

Huduma ya Christians Sharing Christ Film Ministries (CSCFM) ni huduma isiyofungamana na dhehebu lolote, inashirikiana na makanisa mbalimbali na Mashirika yote ambyo malengo yake makubwa ni kuwafikia ambao hawajaokolewa na kuwaleta kwa Kristo na kuwafanya kuwa washirika wa kanisa la mahali. Kwa zaidi ya miaka 40 sasa, CSCFM imeshafanya maonesho ya sinema katika milima, nyika, makao makuu ya miji, na mitaa mbalimbali katika nchi nyingi na sasa huduma hii iko katika mabara 5 ulimwenguni. Huduma ya CSCFM itaendelea kukua na kwenda mahali popote ambapo Mungu atatuongoza na kutuonesha kufika.

MALENGO YETU

"Kuwaandaa, kuwfundisha na kuwasaidia wamisheni wenyeji kusaidia kanisa la mahali kwa kupeleka ujumbe wa wokovu kwa kutumia sinema kwa idadi kubwa ya watu na kwa muda mfupi zaidi"

Maandiko ya msingi: Marko 16:15; Mathayo 24:14; 28:18-20; Luka 24:46, 47; Mdo 1:8; Mdo 11:21, 24, 14:1; Mdo 20:24; 2 Timotheyo. 4:5

Kuandaa, Kufundisha na kusaidia – Huduma ya CSCFM inatumika na kanisa la mahali duniani kote katika kutekeleza agizo kuu la Kristo.

Wamisheni wenyeji –Ni wale wanaofahamu mila na desturi za watu wanaotumika nao na kwa hiyo wanakuwa chachu katika kuwaleta kwa Yesu watu wa nchi yao wenywewe.

Kusaidia kanisa la mahali –Huduma ya CSCFM ni kama kifaa cha mhimu kukturumia katika kulisaidia kanisa la mahali kuwaleta walipotea, kukua katika nguvu ya kiroho na kuongezeka katika idadi pamoja na kuimarisha ushirika mpya.

Kupeleka ujumbe wa wokovu kwa kutumia sinema –Zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani hawajui kusoma na kuandika na hivyo hawawezi kuupata ujumbe kupitia maneno yaliyoandikwa. Mungu ametoa kibali kupitia huduma ya CSCFM kutumia sinema katika kufikisha ujumbe wa wokovu kwa kundi kubwa hili la watu.

Kwa idadi kubwa ya watu na kwa muda mfupi zaidi –Lengo ni kuufikia ulimwengu haraka iwezekanavyo na ujumbe wa kwamba "Yesu ni Njia, kweli na Uzima".

Mungu ametoa kwako nafasi ya ajabu, kupitia huduma ya CSCFM, utapata uwezo wa kuvuna kundi kubwa la roho zilizopotea, kwa kutumia sinema. Asante kwa kuungana na Mungu katika kazi hii ya kuongoza walipotea kwenda msalabani.

FAIDA ZA UINJILISTI WA KUTUMIA SINEMA

"KUWAFANYA WATU WA MATAIFA YOTE KUWA WANAFUNZI":

Agizo la mwiso la Yesu ni lazima liwe wajibu wetu wa kwanza. Mpaka leo lengo limebakia kuwa lile lile: Kumjua yeye kwelikweli katika maisha yetu binafsi na kuuchukuwa ujumbe wake wa upendo na msamaha kwa watu wa ulimwengu huu.

Yesu ni Bwana, wewe na mimi tunao upendeleo wa kuhubiri ujumbe huu hadi mwisho wa ulimwengu uliopotea. Lakini kazi ni kubwa mno! Kila siku, watu katika sayari yetu wanaongozeka kwa haraka zaidi kuliko wingi wa kanisa. Zaidi ya nusu ya watu katika ulimwengu huu hawajui kusoma na kuandika. Katikati ya changamoto kubwa, wachungaji, wainjilisti na viongozi wa tumishi mbalimbali wanaongezeka katika kutumia vyombo kama hivi katika kufikia idadi kubwa ya watu.

Katika vifaa vyote vinavyoppatikana nya uinjilisti, yawezekana hakuna chenye ujuzi au kinachobadilika kama sinema. Sinema inatumika Kama "chujo" kutafuta matunda yaliyoiva ambayo Mungu ameyatayarisha. Kwa miaka mingi nguvu yetu kubwa ya huduma imekuwa ikijulikana kama kwenda nyumba kwa nyumba kutafuta watu amba wanaavutiwa na injili. Lakini sasa katika sehemu mbalimbali vijiji vyote watakuwa wao wenyeewe kuangalia onesho la sinema, na watakuwa na nafasi ya **KUONA NA KUSIKIA** injili hasa ikiwa katika lugha yao wenyeewe. Kwa nini tunatumia vitu nya kuangalia? Kuona ni kuamini! Mikanda ya sinema na aina nyingine ya uinjilisti kwa njia ya kuona huvuta watu wengi, wengi wao hawajui kusoma na kuandika na hawajawahi kungia kanisani wala kusoma Biblia. Tafiti zinazofanya mtu anaweza kukumbuka kwa 11% tu kwa kile alichokisoma na 83% kwa kile alichokional! Kuangalia sinema mara nyingi kwa wiki, inasaidia kuaweka watu katika kukumbuka kwa sababu watu wanaosikia historia ya Yesu Kristo sasa wanaweza kuona kile walichosikia kwa kupitia kuona sinema.

Katika hatua zingine, ikiwa watu na viongozi wa kijiji **WATAONA NA KUSIKIA** ujumbe wa Yesu, kijiji kizima wanaweza kuwa wafiasi wa Yesu. Mara nyingi, wale wanaoitikia wanaweza kufundishwa jinsi ya kukua katika imani na kuwa leta wengine kwa Yesu. Wanaweza kurudi katika kijiji chao kilekile kuwashuhudia watu mambo makubwa Mungu aliywatendea. *Luka 8:39*

Kwa nyongeza kuhudumu kama chujio ni kutafuta tunda lilioiva, uinjilisti wa kutumia sinema unafaida zingine kama zilivyelezwa hapo chini.

Faida ya 1: Sinema ni nyavu za kukamatia roho na kupanda makanisa. Sinema hutumika kama daraja la ushirikiano kati ya kanisa la mahali na huduma ya CSCFM. Maonesho ya sinema siyo kama matukio ya burudani, lakini zaidi kuwasaidia wavuvi (wamisheni) kukamata samaki wengi zaidi (Kuwaleta watu kwa Yesu) kwa kuwapa nyavu za kuvulia (vyombo nya sinema). "*Nifuateni nami nitawafanya kua wavuvi wa watu*". *Mathayo 4:19*

Faida ya 2: Sinema huwafikia watu wasioweza kusoma na kuandika. Zaidi ya nusu ya watu duniani hawajui kusoma na kuandika. Tangu mwaka 1900, wakristo wamechapa zaidi ya Biblia bilion nne, Agano Jipya na Maandiko mengine. Lakini jitihada hizi hazijawasaidia wale ambao hawajui kusoma na kuandika.

Balozi mmoja katika Umoja wa Mataifa alipata kusema kuwa: "Wamisheni wenu wakati mwininge wanafanya makosa. Unaongea kwanza na wanawake na watoto wakati mfumo wa uongozi katika jamii zetu baba ndiye anatambulika kama kiongozi wa familia na mnaleta maandiko mengi. Ni

asilimia 28 tu ya watu wetu ndio wanaojua kusoma na kuandika. Mnaweza kuwafikia kirahisi watu katika nchi yetu kwa kutumia maigizo na sinema."

Sinema inasaidia katika kutafsiri maandiko. Katika maeneo mengi duniani watu bado wanaishi katika utamaduni wa karne ya kwanza – kwa kuvua au kwa kilimo ili kuishi. Wanavaa kandambili, na mtu anayeonekana tajiri ni yule aliye na ng'ombe. Kulikuwa na msisimko wa ajabu pale Yesu alipofanya muujiza wa wa kuvua samaki katika kijiji cha uvuvi cha Filipi. Katika vijiji cha India wanaelewa zaidi pale Yesu alipotumia mfano wa mpanzi. Na Afrika wanaelewa zaidi pale wanapoona Yesu anaponya waliopagawa na pepo wachafu.

Sinema ni kifaa cha mhimi katika kufundishia waumini wapya. Wanaweza kupata uelewa mkubwa wa ujumbe wa Kristo kuitia kuona katika picha za matendo makuu yake, msamaha wake na upendo wake mkuu kwa watu wa kawaida.

Faida ya 3: Karibu kila mtu anaweza kuonesha sinema. Inachukua muda mrefu kumfundisha mwini jilisti kuwa mhubiri mkubwa. Lakini hata mtu ambaye hajui kusoma na kuandika anaweza kufundishwa kwa muda mfupi akajua kuonesha sinema. Kama timu za sinema zinavyoweza kupatikana na kufundishwa, ina fanana kwa ukaribu na kuwa na mamia ya safari za Billy Graham alizosafiri duniani kote akieneza kujumbe wa injili.

Faida ya 4: Sinema inalazimisha usikivu. Sinema inakusanya watu wengi na kuwavutia wale ambao yawezekana hawajawahi kuhudhuria mkuutano wa injili au ibada za kanisa za kawaida. Sinema inayo oneshwa katika lugha ya kuzaliwa inaeleweka zaidi. Moja ya faida kubwa ya mikanda ya sinema ni kwamba inapatikana katika lugha nyingi. Katika saa moja au mbili watu wanaweza **KUONA** na **KUSIKIA** ujumbe rahisi wa kristo katika lugha yao wenywewe. Mungu tayarai anatayarisha miyo katika ulimwengu wote, na watu wengi wanaitikia pale wanapoolewa zaidi mpango wa mungu wa wokovu katika maisha yao.

Kwa historia hii, tuendelee sasa katika hatua zinazohusika na upangaji wa onesho la huduma ya sinema lenye kuleta matunda.

MATAYARISHO NA UPANGAJI

MAOMBI NA MPANGO:

Anzisha kikundi cha maombi. Muombe Mungu kwajili ya Maono. Endelea kuomba kwamba Roho Mtakatifu aleta watu wengine kushirikiana nawe. Malengo mazima ya uinjilisti wa kutumia sinema ni kuwafikia watu amba hawajaokolewa na kuwaleta kwa Yesu na kuwafanya kuwa washiriki wa kanisa la mahali au katika kupanda kanisa jipya.

Tambua kanisa mwenza wako au taasisi ya kidini lazima ihusishe viongozi mhimu.

Je, kanisa au taasisi hiyo inataka kupanda kanisa jipya la nyumbani, kukuza kanisa liilopo, au yote mawili kwa pamoja?

Je, kanisa au taasisi hiyo itatoa washauri waliofundiswa?

Je, kanisa au taasisi hiyo itafanya ufuatiliaji kwa wale waliookolewa?

Je, Kanisa au taasisi itatoa maandiko kama vile Biblia, Agano Jipya, na traksi

Tumia ramani ya nchi yako, gawanya kata, wilaya, mikoa katika kanda. Kila kanda ni lazima iwe na wilaya 1 hadi 10 au mikoa (**Kiambatanisho na. 9 na 10**) kwa kuanza, lengo letu ni kuwa na timu moja katika kila kanda. Lengo la baadaye ni kuwa na timu nyingi katika kila kanda. Kila Mkurugenzi wa nchi wa huduma ya CSCFM atahitaji kupanga ukubwa wa kila kanda. Ukubwa wa kanda unategemeana na wingi wa watu, jiografia ya nchi (tambalale, milima, mito/maziwa) vikwazo vyta kiserikali, n.k. Kila kanda lazima ifanye kazi kwa ufanisi, kwa kutengeneza orodha au kwa kuonesha kwa mpango (kwa kutumia rangi mabalimbali). Hii njia pia inaweza kutumika katika kugawanya majiji makubwa. Jinsi timu zitakavyokuwa zikiongezeka, kila kanda inaweza kugawanyika tena ili kuleta ufanisi wa utendaji wa kazi.

Mara tu ya kukamilika ramani hii kugawanywa katika kanda, ni lazima iwekwe ukutani nyumbani mwako, ofisini, au kanisani. Itatumika kama kikumbushio katika kuombea eneo lako la huduma.

KUCHAGUA ENEO LA KUFANYIA ONESHO LA SINEMA:

Angalau inashauriwa kuwa ndani ya kanisa.

Kama kuna kanisa mwenyeji, inashauriwa kuwa na onesho la sinema angalau mita 200-300 kutoka kanisani. Watu wengi hawana uhuru wa kuingia kanisani kutokana na matatizo yao binafsi (imani mabalimbali au dini), kwa hiyo ni vizuri kuweka onesho la sinema katika eneo la wazi mbali kidogo na kanisa (Luka 5:4), kama vile uwania wa mpira, maeneo wazi ya jamii, ukumbi wa jamii, kiwandani, shulenii n.k. Siku inayofuata, waumini wapya wanaweza kuelekezwa kanisani kwa ufuutilaji kutokana ka kukata shauri kwao.

Kama hakuna kanisa karibu na mahali pa onesho, lengo kubwa ni kupanda kanisa. Makanisa mengine yanaweza kukupa ruhusa ya kutumia majengo au sehemu zao za kukutania. Ikiwa ni nyumba moja tu au mbili zina umeme eneo lile, labda watu hawa wanaweza kutiwa moyo na kuwaomba kuwa wenyeji wa onesho la sinema na umeme wa kutumia unaweza kutoka nyumba zao ikiwa hakuna genereta.

Kama sinema inafanyikia kijijini ambako hakuna umeme ni vizuri kufikiria eneo la kilometra kama 9 hivi na onesho likafanya katikati ya eneo hilo ili watu wasitembee kwa umbali mrefu kuja kuangalia sinema.

Tumia ramani kuelezea maeno ambayo unapanga kuyafikia na sinema. (**Kiambatanisho na. 9 & 10**).

KUOMBA KIBALI CHA ONESHO LA SINEMA

JINSI YA KUOMBA KIBALI CHA ONESHO LA SINEMA KWA VIONGOZI WA SERIKALI KATIKA ENEO HUSIKA

Angalau tuma maombi yako wiki moja kabla ya onesho, weka ratiba ya kukutana na kiongozi wa serikali katika eneo husika kupanga naye jinsi ya onesho litakavyokuwa na mahali ili uwaeleze mpango wako wote wa onesho. (*Klambatanisho na.14*) Ikiwezekana, ongozana na mtu (mchungaji wa kanisa mwenyeji), Mshirika yeoyote anayeaminika, au kiongozi yeoyote wa kanisa mwenyeji) kutoka eneo husika, katika kukutana na kiongozi wa serikali. Onesho la cinema lazima likubaliwe au lihakikishwe na viongozi wa serikali katika eneo husika ambapo ruhusa yao itakuweka huru zaidi wakati wa onesho.

Kuwa mpole na mnyenyekevu.

Baada ya kujitambulisha mwelezee lengo lako la kuwa pale kwa ufupi

Mwelezee aina ya cinema uliyoipelea pale.

Kuwa na ratiba ya tarehe mbalimbali na sehemu mbalimbali za maonesho ili kiongozi huyu wa serikali awe na uhuru mpana wa kuchagua ifanyike lini na wapi.

KUFUNDISHA TIMU YAKO

Kuwa makini katika kufundisha wajitolea watatu au wanne kutoka katika kanisa mwenyeji au taasisi kwa kila kata, wilaya, jimbo na mkoaa ndani ya kanda watakao kusaidia kuwasiliana na makanisa na viongozi wa serikali katika maeneo husika kwaajili ya maonesho ya sinema katika maeneo hayo.

Washiriki katika timu lazima wawe tayari kufanya kazi pamoja, wakisaidiana katika kuleta ufanisi wa kazi zao. Timu yote ni lazima waelewe kuwa katika jithihad za uinjilisti lazima kuwe na upinzani wa shetani na kwa sababu hii, kila mwana timu lazima awe tayari kutembea katika imani, kujitoa kwa Roho Mtakatifu, na awe na mwito wa kufanya kazi ya Bwana.

WAONESHA SINEMA NA MAJUKUMU YAO:

Mshereheshaji Mkuu: (Mara nydingi huwa kiongozi wa timu [wewe])

Kutana na wanatimu wenzako kwa maombi na maelekezo ya mwisho! Kabla ya onesho kuanza, tenda kama mratibu wa onesho.

Wasiliana kwa ukaribu na kanisa mwenyeji au kiongozi wa serikali wapi onesho litafanyikia (tarehe, mahali, na muda ulioruhusiwa kutumika kwa onesho).

Chukua mahudhurio ya onesho zima na idadi ya watu waliompa Kristo maisha yao na wakaongozwa sala ya toba na kupewa maelekezo na kiongozi wa timu au mchungaji kwa ufuutiliaji.

Mara tu ya onesho kuisha, mshereheshaji mkuu au mchungaji wa kanisa mwenyeji lazima atoe mwaliko (***Kiambatanisho na. 11, 12, na 13***)

KUTAMBULISHA mkanda. Katika kutambulisha mkanda isichukue zaidi ya muda wa **DAKIKA MBILI**. Nilazima ijumuushe na shukrani kwa kanisa mwenyeji, sababu (maudhui) ya mkusanyiko, na maelezo ya kitakachofanyika wakati wa hitimisho la sinema.

Kabla ya kuanza Onesho, mzungumzaji, au mchungaji wa kanisa mama lazima aseme, "wakati wa kubadilisha mkanda, tafadhari bakia mahali ulipo kwa muda wa dakika 5 nasi tutakueleza jambo mhimi".

KUTUNZA KUMBUKUMBU (tutaliongelea baadaye)

Washiriki katika timu: (waumini wa kanisa au taasisi mwenyeji watakao amua kutoa ushuhuda (inawenza kuruhusiwa au kutokuruhusiwa)).

Ushuhuda uwe wa dakika 3-5

Kama kuna watu wengi zaidi wanaotaka kutoa ushuhuda, maridhiano lazima yafanyike kwa kiwango cha kupendeza.

Mwendeshaji sinema: (Huyu mara nydingi huwa kiongozi wa timu au mzungumzaji [wewe])

Vyombo nya sinema kutoka huduma ya CSCFM huja kwa malengo ya kufanya uinjilisti wa nje na **SIYO** kwaajili ya matumizi ya ibada ya kanisani au matangazo ya mtu binafsi au kwa kazi ye yeyote inayofanana na hiyo.

Hutayarisha vifaa vyote vinavyotakiwa kwa safari kwenda kuonesha sinema.
(Kiambatanisho na. 16)

Haishauriwi kuchukuwa Mikanda yote kwenda nayo katika kila onesho, mkanda 1-2 inatosha sana kwenda nayo katika onesho moja kwa sababu inaweza kuibowi.

Jinsi ya kutunza na kusafisha DVD: Unapojiandaa kusafisha DVD, ni muhimu ukajua jinsi ya kuilinda. Usiguse eneo linalong'aa badala yake pitisha kidole chako katikati ya tundu kisha vidole vingine viguse kwenye mzunguko kwa nje. (Mfanu, ingiza kidole chako kikubwa katika tundu la katikati na vidole viliviyobaki viguse pembedni. Unaweza pia kushika kwa kuzunguka mduara wa nje kwa kidole kikubwa kugusa upande mmoja na vinavyobaki eneo lingine kwenye mzunguko wa DVD. Kusafisha tumia kitambaa laini na maji, tumia sabuni ya maji ya mtoto mchanga (au aina nyininge ya sabuni ya maji). Chovya kitambaa chako cha laini katika sabuni ya maji. Anza kuifuta DVD yako kwa kuanzia eneo la katikati ukielekea nje kwa mzunguuko ulio sawa. Endelea kufanya hivi mpaka DVD inapokuwa safi na imekauka kabisa.

Funga na jaribia vyombo vyako angalau dakika **60** kabla ya kuanza onesho. Hakikisha kwamba waya zako zote zimechomekwa katika matundu husika.

Kaa karibu na projekta wakati wote wa onesho ili kulinda vifaa ikiwa kutatokea shida ya aina yoyote! zima taratibu na kwa makini taa (balbu) zako baada ya onesho ili ziweze kukaa na kutumika kwa muda mrefu zaidi.

Kichuja hewa (kichuja vumbi) kilichoko kwenye projekta, ni lazima kisafishwe (tumia maji na sabuni ya maji – Usitumie kemikali) kila baada ya maonesho 3-4.

Kumbuka: Baadhi ya projekta hazina vichujio nya hewa au vumbi

Huveka kila kitu katika mpango na kurudisha vifaa nyumbani/ofisini au katika sehemu salama mara tu ya onesho. USIRUHUSU vifaa kubaki ndani ya gari usiku mzima kwa sababu vinaweza kuibowi. Pia jua kuwa joto linaweza kuharibu projekta na CD au DVD.

VITU AMBAVYO HUTAKIWI KUFANYA WAKATI WA ONESHO:

Kuiacha projekta bila mtu wa kuiangalia.

Kuongea na simu wakati mkanda unaendelea.

Mzungumzaji: Mara nydingi huwa kiongozi wa timu au mzungumzaji [wewe]

Maelezo ya ufunguzi ni lazima yasadie kuimarisha mahusiano na watazamaji. Ongea kwa kukumbuka makundi ya watu na kile kinacho wavutia kila kundi.

Kabla ya kuanza Onesho, mzungumzaji au mchungaji wa kanisa mwenyejji lazima aseme, " Wakati wa kubadilisha mkanda, tafadhari bakia mahari ulipo kwa takribani dakika 5 nasi tutakujulisha kinachoendelea".

Mwisho wa Onesho, mzungumzaji atatoa mwaliko wa kumpokea Kristo. (**Kiambatanisho na. 11, 12 & 13**)

Mzungumzaji na washauri nilazima wagawe na kuzikusanya kadi za ufuatiliaji (**Kiambatanisho na. 18**) kwa wale waliokuja mbele wakati wa mwaliko.

Maneno ya kufunga Onesho lazima yawe mafupi na ya kuelewaka, ongea neno la shukrani kwa kiongozi wa serikali aliywakaribisha au kanisa mwenyeji kwa kuwaruhusu kuwepo mahali pale.

Mzungumzaji huandika kumbukumbu za mahudhurio ya watu na wale waliompokea Yesu kwenye sinema. Angalia fomu ya ripoti ya mwezi ya CSFM (**Kiambatanisho na. 20**)

washauri: (Hawa mara nyingi huwa mchungaji na washiriki kutoka katika kanisa au taasisi mwenyeji)

KABLA YA ONESHO LA SINEMA:

Kufundisha washauri katika kila onesho la sinema ni mhimu na inaleta utofauti kati ya huduma ya sinema na sinema ya kuburudisha. Washauri ni lazima wafundishwe kutoka katika kanisa au taasisi mwenyeji wa onesho

Washauri hawa ni lazima wawe wako tayari kuongea habari za Kristo na watu wengine. Ni lazima wafundishwe jinsi ya kutumia Biblia au traksi kutafsiri injili kwa wale wanaopita mbele baada ya kumpokea Kristo katika onesho.

Kuwafundisha hawa viongozi huchukua masaa kadhaa ni vizuri mafundisho kufanyika kabla ya onesho la sinema. Ni vizuri wanafunzi wote wakapewa nafasi ya kujaribia jinsi watakavyoshuhudia kama njia mojawapo ya mafunzo. Angalia fomu ya taarifa ya mwisho wa mwezi ya CSCFM (**Kiambatanisho na. 20**). Namba ya watu hawa inatakiwa kuandikwa katika chumba kilichoandikwa **idadi ya watu walipata mafunzo ya uinjilisti**.

Sehemu moja ya mafunzo lazima isisitize kuwa tunaweza kuwa washuhudiaj wazuri kama tunajazwa na kuungozwa na Roho Mtakatifu. Na pia ni mhimu kwa washauri kuelewa kuwa ushuhudiaji wa mafanikio ni ule wa kuwaeleza watu habari za Kristo katika nguvu ya Roho Mtakatifu na kuacha matokeo kwa Mungu.

WAKATI NA BAADA YA ONESHO LA SINEMA

Kuwachanganya baina ya watazamaji na kuimarisha mahusiano na kuwaweka katika sehemu tulivu.

Baada ya onesho la sinema na mwaliko wa injili, washauri lazima wawe wametayarishwa kutoka mbele mara moja ili kusaidia kuwatia moyo watu wengine kufuata. Wakati huo, washauri lazima wawe wametayarishwa kuwapokea wale waliokuja mbele na shauku ya kupata maelekezo zaidi au kuelekezwa jinsi ya kumpokea Kristo kama mwokozi wao.

Mzungumzaji na washauri lazima wagawe kadi za ufuatiliaji kwa wale waliokuja mbele wakati wa mwaliko. (**Kiambatanisho na. 18**) kujibu maswali; kuwaongoza katika sala ya toba na kuwatia moyo kuhudhuria kipindi cha ufuatiliaji katika kanisa la mahali au katika sehemu yoyote iliyoteuliwa kufanyikia. Inashauriwa kuwa kila mtu aliyekata shauri lazima apewe (Kama zinapatikana) traksi, Agano Jipy, au Biblia.

Wakati onesho linapoisha, ni jambo la msingi sana kuomba kwaajili ya waumini wapy, waeleezee uhakika wa wokovu, ongea nao kuhusu maisha mapya katika Kristo na kuwatia moyo kuwa kiungo katika mwili wa Kristo kwa kuijunga na kanisa la mahali na kuhudhuria mafundisho ya Biblia ya kikundi.

ONESHO LA SINEMA

MATANGAZO (siku 2-5 kabla ya tukio):

Madhumuni na malengo mazima ya kutumia propaganda ni kwamba watu wote, katika eneo liliokusudiwa, watajua, wapi na wakati gani sinema itakuwepo na kuendelea, na kwamba kila mtu amealkwa kuhudhuria.

Lisome eneo na elewa aina gani ya matangazo inaweza kuvutia watu katika utamaduni wao. Muombe Mungu akupe watu wanaofaa na usafiri ili kufikia njia uliyochagua katika kutangaza.

Mabango yaliyochapwa (matangazo), na vipeperushi yanafaa sana kama msaada kualika watu kufika katika onesho la sinema. Haya yanaweza kusambazwa mlango kwa mlango na mwaliko binafsi, au yanaweza kubandikwa kwenye maduka, vioski, miti na sehemu zote za mikusanyiko katika eneo husika. (*Kiambatanisho na. 19*)

Radio na Magazeti

Magari yaliyofungwa vipaza sauti pia yanaleta hamasa katika kutangaza onesho la sinema.

Kuwa mbunifu jinsi ya kulifika eneo lengwa na matangazo kabla ya onesho la sinema. Buni njia mpya zitakazo gusa hisia za watu na kuhamasisha

KAZI (Siku ya tukio):

Funga vyombo vyako mapema. Vjaribie mapema ili kama kuna tatizo lipate ufumbuzi mapema. Muda mfupi kabla ya kuanza onesho, wavutie watu kufika eneo la sinema kwa kutumia kikundi cha uimbaji, kupiga kanda za kwaya na mapambio kwa kutumia vipasa sauti.

Kusanya timu yako na washauri waliopata mafunzo kukumbushana kipi kitafanyika wakati wa onesho, pia ombo;

Kwa watazamaji kuokolewa

Kwa vyombo kufanya kazi vizuri mpaka mwisho wa onesho

Kukemea shetani na hila zake zote za kuharibu onesho la sinema

Waoneshe washauri mahali pa kusimama wakati wa kushauri wakifuata mkanda unavyoelezea.

Watume washauri/ washiriki wa kanisa kwenda mitaani kugawa matangazo au mabango na kuwaalika watu kufika katika onesho la sinema.

Wasiliana na washauri wa kanisa mwenyeji muda na mahali patakapofanyika mkutano wa ufuatilaji hivyo wanaweza kuwaambia watu wale waliompokea Yesu kwa kufuatilia mkanda.

MATATIZO (UTATUZI) – ya kutarajia na yasiyo ya kutarajia:

Sio kila onesho linakwenda vizuri, wakati mwagine kuna matatizo yanatokea, hapa kuna ushauri karibu katika maeneo yote.

Hali ya hewa mbaya: Uwe na eneo lingine liochaguliwa tayari ikiwa Hali ya hewa mbaya itakufanya usiweze kufanya onesho nje. Hii inaweza kuwa kwenye darasa la shule au ukumbi wowote ulioko karibu. Beba mwamvuli au turubai wakati wa masika. Kama mvua siyo kubwa sana, unaweza kuifunika projekta tu na onesho likaendelea.

Kuharibika kwa kifaa: Kama kifaa kitaharibika na uwezo wa kikitengeneza ukawa mgumu wasimulie watu mambo yaliyoko katika mkanda na wakati wa kufunga toa mwaliko. Wape washauri kutoa ushuhuda na tangaza siku nyininge utakayooneshaa sinema.

Kibali kusitishwa: Kama umeamuliwa kuondoka kwa kibali chako kusitishwa panga kufanya onesho lako katika kiiii au ene la iirani na hapo ulipokataliwa.

Kuwepo na taa yenyenye mwanga mkali katika eneo la kuoneshea sinema : Tumia pouzo ndefu, funika taa ile na nguo nzito nyeusi.

SASA TUKO TAYARI KUONESHA STNEMA

Vyombo vya huduma ya CSCFM ulivyopewa ni kwaajilli ya huduma ya uinjiliisti wa nje TU

na HAVIBUHUSIWI kutumika katika ibada za mikutano ya kanisani au katika

Matangazo ya aina yoyote binafsi!

UFUATILIAJI

Hii ni sehemu ya pili ya mhimu katika Onesho la sinema:

Mchungaji na washiriki wa kanisa mwenyeji lazima waelewe kuwa jukumu la ufuatiliaji linaangukia katika mabega yao kama huduma ya CSCFM ilivyo kifaa cha kusaidia kanisa la mahali.

Wana timu nawashiriki wa kanisa mwenyeji ni lazima wafundishwe kama watoa nasaha na ushauri kwa watu wapya wanaowafanya ufuatiliaji. Hii sababu ya mhimu inayoleta utofauti kati ya unjilisti wa kutumia sinema na kuonesha sinema.

Kwa ufupi, ufuatiliaji wa matunda yaliyotokea kutokana na kuonesha sinema inajumuisha:

Mwaliko mzuri unaoeleweka

Washauri waliokazini na tayari, wanatoa mapokezi ya ukarimu kwa watu wanaokuja mbele wakati wa mwaliko.

Kutoa traksi za injili, Biblia, au Agano jipya.

Kukusanya majina na anuani kwaajili ya mwendelezo wa ufuatiliaji.

Kuomba na waumini wapya

Kutangaza mkutano wa ufuatiliaji wa mwanzo kabla ya waumini wapya hawajaondoka katika eneo la sinema ndani ya masaa 48, kama inawezekana,

Asubuhi inayofuata washauri watembelee nyumba zote kuhakikisha watu waliompokea Yesu jana yake. Hakikisha kwamba watu waliompokea Kristo wanaufatiliwa kikamilifu (**Kiambatanisho na. 18**) kwanza na baadaye wale wanaotamani kupata maeleo zaidi au kuhudhuria mafundisho ya Biblia. Hii inamaana zaidi ikiwa unafanya onesho katika eneo ambalo tendo la watu kupita mbele linaweza lisifanyike kwa uwazi kwa sababu ya vipingamizi vyta mila, dustui na mapokeo ya watu wa pale.

KUTUNZA KUMBUKUMBU

KUMBUKUMBU KWAAJILI YA KUTUMA RIPOTI KATIKA HUDUMA YA CSCSFM:

Taarifa zinazotakiwa:

Tuma taarifa yako kwa kupitia tovuti ifuatayo www.christianssharingchrist.org si zaidi ya tarehe 5 ya mwezi unaofuata!! Tumia fomu ya taarifa ya kila mwezi ya huduma ya CSCFM (*Kiambatanisho na. 20*) tunza matukio ya kila siku na ya mwezi ya maonesho ya sinema, taarifa ambazo zitahitajiki kila mwisho wa mwezi. Unaweza kutumia fomu hii kutunza kumukumbu zako mpaka pale utakuwa tayari kuzituma kwa mtandao kwa huduma ya CSCFM.

- 1 – Idadi ya maonesho yaliyofayika
- 2 – Idadi ya watu waliohudhuria
- 3 – Idadi ya watu waliompokea Kristo
- 4 – Idadi ya traksi zilizogawiwa
- 5 – Idadi ya Biblia/ Agano Jipya zilizogawiwa
- 6 – Idadi ya kozi za uinjiliisti zilizofundiwa (KWA AMERIKA YA KATI TU)
- 7 – Idadi ya watu waliopata mafundisho ya uinjiliisti
- 8 – Idadi ya makanisa au makunid ya nyumbani yaliyopandwa

Maonesho ya sinema: Inatakiwa kuwa kila timu ya huduma ya CSCFM ifanye kwa uchache maonesho 8 kila mwezi **au** jumla ya maonesho 96 kwa uchache kwa kalenda ya mwaka mzima. Katika kila mwisho wa robo ya mwaka kila timu itafanyiwa tathmini ya maendeleo yake, na ikiwa chini ya maonesho yanayotakiwa utajulishwa na mkurugenzi wako wa nchi.

Kwa nyogeza katika utumaji wa taarifa kwa kila mwezi kupitia mtandao, huduma ya CSCFM ingelipenda kupokea shuhuda fupi zinazoleweka za maandishi (**Kiambatanisho na. 15 – mfano wa shuhuda**) za matendo makuu ya Mungu, miujiza ya Mungu; wakati unasafiri **kuelekea au kutoka na kabla ya safari, wakati wa safari, na baada ya onesho la sinema.** Picha na matukio na labda mikanda ya video vinakaribishwa kwani picha na mikanda inatusaidia katika kuongea na watu juu ya kazi za huduma ya CSCFM na wafadhiri wetu. Hivi vyote lazima vitumwe kwenye barua pepe ifuatayo cscreport@aol.com.

Kumbuka: Shuhuda na picha Mara zinapopokelewa zinatumwa kwa watu wengi wanaofadhiri huduma yetu na kwa watumishi wa Mungu katika huduma yetu duniani kote, kwaa jili ya kutiana moyo ambapo zinasaidia pia kuongeza ufanisi na ufadhiri katika huduma yetu ya CSCFM. Kwa siku zijazo, kutakuwa na ongezeko la nafasi katika fomu za taarifa kwenye tovuti yetu ya www.christianssharingchrist.org nafsi ambazo zitakusadia kuweka picha, shuhuda, na maombezi ya mahitaji. Mara hilli litakapokamillika, hutaendelea kutuma picha, na shuhuda katika barua pepe yetu ya cscreport@aol.com.

Kwa matumizi yako – Inasaidia ingawaje SI mhimu kutuma pamoja na taarifa ya kila mwezi:

- 9 – Jina la kanisa mwenyeji
- 10 –Eneo la mji/ kijiji onesho lilikofanyika
- 11 – Lugha ya mkanda uliooneshwa
- 12 – Tarehe ya onesho la sinema

KUMBUKA: KAMWE usikadirie au kubuni. Uhakika na uaminifu ni mhimu zaidi kuliko namba kubwa ya idadi ya watu.

**** Hakuna ujazaji wa taarifa kila mwezi utaleta kutokupokea msaada au msaada wa baadaye. ****

(HAKUNA RIPOTI, HAKUNA MSAADA!)

MAELEKEZO YA UJAZAJI WA TAARIFA

KWA KUTUMIA MTANDAO

Maelekezo ya Jumla:

Kila mwezi unapoisha, kiongozi wa timu atatumwa taarifa za mwezi zinazotakiwa moja kwa moja Marekani kwa kutumia tovuti ya Christians Sharing Christ. Mkurugenzi wa nchi atakuwa na uwezo wa kuona moja kwa moja taarifa za nchi yake mara tu zinapoingizwa katika tovuti.

Kila timu itakuwa na jina tofauti na timu nyiningine la kutumia katika kuingiza taarifa hizo na namba zake za siri ambazo zitatumika katika kuingia kwenye mtandao wa huduma ya Christians Sharing Christ. Jina la utambulisho pamoja na namba za siri utapewa. *** **MUHIMU***** Majina yote ya utambulisho na namba zake za siri ni jambo la maana sana kwa maana hiyo yanatakiwa kujazwa kwa usahihisi katika tovuti ya huduma ili uweze kungia. (**Kiambatanisho na. 2**) *Unapoipata hizi, ziandike kama inavyooneshwa hapo chini*

Jina lako la utambulisho _____

Namba ya siri _____

Kuingiza taarifa kwa kutumia tovuti ya CSCFM:

Ingia katika mtandao wa huduma ya CSFM kwa kutumia tovuti ifuatayo <http://www.christianssharingchrist.org> (**Kiambatanisho na. 1**)

Bonyeza mahali palipo andikwa **Enter Missionary Area**. Kitatokea kisanduku kidogo kwaajili yako kuingia

Baada ya kuingiza jina lako la utambulisho na namba za siri, bonyeza mahali palipoandikwa **login**. Kama utakuwa umeingiza taarifa zako vizuri, fomu ya kujaza taarifa itatokea, vinginevyo, ujumbe wa kukosea utatokea na unaweza kujaribu tena. (**Kiambatanisho na. 3**)

